

# DESIGNER SIGNS

Extracted from TIME FOR A SIGN
By: M. P. Esmail

Japokuwa alama au ishara ni vitu muhimu sana katika maisha yetu ya kila siku, lakini pia ni vitu visivyotiliwa maana katika maisha yetu. Mbali na matumizi yake tofauti na matumizi mengine yasiyo na hesabu, alama au ishara ni vitu muhimu hasa kwa usalama wetu. Tunahitaji alama mbalimbali ili zitufahamishe tusiyoyajua tuyafahamu na wakati huo huo mwonekano wa hizo alama uwe unaochochea na kuipa mwonekano mzuri miji na majiji yetu.



Alama au ishara ni muhimu sana maana kukosekana kwa njia sahihi za alama au maelekezo ya kukujulisha jinsi utakavyoweza kufika katika duka unalotaka kwenda kununua bidhaa; hali kadhalika, kutakuwa na mkusanyiko mkubwa katika maeneo ya biashara za rejareja kama watu wange jiendea tu bila maelekezo duka fulani liko mahali gani, kama ilivyo kwamba kungekuwa na vurugu na misongamano isiyo na sababu kama barabara zisingekuwa na alama za barabarani za kukuongoza upite upande gani au usipite barabara hiyo. Hata kama mtu angelihitaji kwenda sehemu ya karibu tu ingekuwa tabu. Katika nyakati tulizo nazo, mtu hawezi kufika stendi ya mabasi bila kuwa na maelekezo au alama zitakazo waelekeza abiria jinsi ya kufika huko na kudhibiti wasafiri walio kituoni, au kuendelea kuweka kumbukumbu zao kwa kutumia njia zile zile za kawaida au mabango ya kieletroniki.




Kila mara tunaletewa kanuni mpya na miongozo na utekelezaji wake kwa alama zinazohusisha rangi, umbile, ukubwa, ukubwa wa herufi zilizotumika kuandikia tangazo lenyewe, jinsi tangazo linavyotakiwa kung'aa na aina ya mng'ao uliotumika, na kadhalika. Kuna vitu na vigezo mbalimbali vinavyotiliwa maanani ili alama ziweze kuonekana vyema, kusomeka, na kutafsirika kwa ufasaha ili mara moja ziweze kutoa ujumbe uliokusudiwa.

Hivi sasa ni lazima kwa kila chombo cha umma cha usafiri - iwe ndege kwa usafiri wa angani au meli au hata nyambizi kwa usafiri wa majini - kuwa na vitu ama ishara za usalama wakati wa kujiokoa, zilizotengenezwa kwa vitu vinavyong'aa. Kama kuna ishara au alama ya kawaida tu ya kuonesha mlango wa "kutoka", inaweza ikaokoa maisha kutokana na janga la kifo linalokabili - kwamba kunapotokea tatizo la kujiokoa, mtu ataamua haraka kutumia mlango wa "kutoka" ili ajiokoe, lakini kama alama kama hiyo haipo kunaweza kukasababisha kifo. Hapo tunaweza kuona jinsi inavyoweza kufanya tofauti kati ya maisha na kifo.

Wakati huo huo, kutakapokuwa na alama iliyotengenezwa kwa ustadi na kimadaha, inayoelekeza sehemu ya juu ya jengo moja kuwa kuna biashara, inaweza kuwa kivutio tosha cha biashara, tena usichokitarajia. Hii maana yake ni kwamba maisha bila ya kuwa na alama au ishara ni wazo lisilofikirika kabisa.

Lakini mbali na matumizi yake ya kawaida, siku hizi watu wanazifurahia mno alama au ishara kwa jinsi zilivyotiwa nakshi na mapambo mbalimbali ya kuvutia. Kuwa na alama zilizotengenezwa kwa usanifu wa hali ya juu ili ziweze kuzidi kuwa na jinsi zinavyoweza kubadilisha mandhari ya eneo yanayolizunguka; kuwa na mvuto na mwonekano wa aina yake unaoleta mng'aro laini huku ikiwa rahisi kupata, mahitaji yake yanaendelea kuongezeka kila uchao.

Si rahisi kusema kuwa alama za siku hizi hazihesabiki tena kuwa hazifanyi kazi, bali ndizo zilizogeuza sura mbovu za majengo yasiyofaa katika baadhi ya maeneo ya mijini kuwa ya msisimko, huku yakileta mvuto katika maeneo ya sehemu za kazi na kuzifanya sehemu za mijini kuwa za kuvutia.

Kwa maoni yangu, alama sasa zinaweza kuhesabika kama sehemu ya tasnia ya mitindo ikijenga "Utamaduni Mpya wa Alama" ambao ndiyo unaonifanya mimi nipende kuuita utamaduni wa "Alama za Usanifu", kama vile tulivyo na mavazi ya wasanifu, mikoba ya kina mama au kina baba, manukato (pafyumu), viatu, miwani ya jua, na hata kalamu, kwa hiyo kwa nini hivyo kusiwe kwa "Alama za Usanifu?"

Wakati uliopita, alama zilikuwa zikitengenezwa na mafundi stadi waliokuwa wakitumia vifaa vya kawaida vya mikono, lakini kuja kwa maendeleo ya teknolojia, tasnia ya alama kwa ujumla imegeuza kwa haraka kutengeneza 'Alama za Wasanifu' wanaotumia mashine za kisasa na walio na ujuzi wa hali ya juu, ambao wamekuja na mitindo ya kustaajabisha kabisa ambayo si tu inatoa ujumbe au kutoa maelekezo, bali pia kuleta mvuto kwa watumiaji alama hizo. Wasanifu hao ni kama vile wanazungumza na sisi tunapoangalia kazi zao, kama vile maua yanavyozungumza na mtunza bustani mahiri wa kazi yake wakati maua hayo yakimvutia mtazamaji wakati anapoyaangali. Kwa hiyo tasnia ya alama imekuwa ni tasnia ya mabilioni ya dola iliyoenea duniani kote. Na kutokana na maendeleo ya kiteknolojia ya kidigitali, tasnia hii imekuwa na uchangiaji mkubwa kwelikweli wa maendeleo haya.



Hapa ndipo Sign Industries Ltd inapojitokeza. Tumeendelea kujizatiti kwenda sambamba na viwango vinavyokubalika duniani katika teknolojia, vifaa na mitindo yenyewe. Huwa kila mara tukirekebisha mashine zetu na vitendea kazi vingine, na tumetumia nafasi hiyo kujitangaza kimataifa, huku tukiendelea kwa muda mrefu sasa katika tasnia hii ya usanifu. Usanifu tunaoufanya na vitu tunavyovitengeneza vinatokana na jinsi tunavyoguswa binafsi, na hivyo, kutuwezesha kutengeneza vifaa vilivyo na hisia za kisanaa. Kazi zetu zitakufurahisha na kukupa msukumo na msisimko na pia kuongeza uzuri wa mwonekano mpya ndani ya moyo wako.

Tunakukaribisha utembelee ukumbi wetu wa kisasa tunakooneshea bidhaa tunazoziuza, ambako utapata karibu kila kitu utakachohitaji na hata zaidi yake, vyote vikiwa vimeoneshwa katika hali itakayokuridhisha na kukufaa sana – kuanzia duka la nguo na urembo na mambo ya ulimbwende, maelezo ya mitindo ya mavazi, alama za barabarani, utaratibu wa vibao vya majina, maelezo ya watu mashuhuri, na kuonesha uwezo wetu wa hali ya juu katika usanifu, na sehemu yetu ya DIY utakavyoweza kujionea mwenyewe jinsi watu wetu wanavyojituma – yote hayo yakionesha uteuzi wetu mpana wa kila aina ya mitindo ya usanifumajengo katika mazingira ya pamoja au yatakayoendana na vionjo vya wahafidhina wanaioishi mijini au mbadala wa aina ya vitu unavyovipenda ama hata visivyo vya kawaida.

Maelezo zaidi yanapatikana katika tovuti yetu, na ushauri na taarifa zaidi zinaweza pia kupatikana kupitia barua pepe. Kama huna uhakika kwa kile unachokitaka au kama unahitaji ushauri wa kitaalamu, wasiliana nasi kupitia kitengo cha huduma za ushauri. Angalia sehemu ya "Ushauri".

Mahboob Esmail
C.E.O. - Sign Industries Ltd,